**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA SIKU YA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI 2022

**UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE (JINCC),**
**DAR ES SALAAM**
**TAREHE 7/7/2022**

*Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo;*

*Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (Mb.), Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar;*

*Mheshimiwa Prof. Matsie Angelina Motshekga, Waziri wa Elimu ya Msingi wa Afrika ya Kusini;*

*Waheshimiwa Mawaziri mliopo;*

*Waheshimiwa Mabalozi na wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa hapa Tanzania;*

*Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mama Kate Kamba, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mheshimiwa Pauline Gekul (Mb.), Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; na Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote mliopo;*

*Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Makatibu Wakuu wote mliopo;*

*Ndugu, Yakub Saidi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Naibu Makatibu Wakuu wote mliopo;*

*Prof. (wa Kiswahili) Aldin Mutembei wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wahadhiri wa Ngazi mbalimbali na Wadau wote wa Kiswahili;*

*Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mkoa wa Dar es Salaam,*

*Wakurugenzi wa Wizara na Makatibu Watendaji wa Taasisi za Wizara;*

*Waheshimiwa Viongozi wetu wa Dini mbalimbali mliopo;*

*Wafanyakazi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (SMT na SMZ) pamoja na wafanyakazi wa BAKITA na BAKIZA;*

*Vikundi vyote vya Burudani (Washairi, Wanne Stars, TaSuBa na Brass Band);*

***Waandishi wa habari;***

***Wageni waalikwa kutoka ndani na nje ya nchi,***

***Mabibi na Mabwana;***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania………Habari za Asubuhi!**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na Fadhili, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufika siku ya leo na kuungana na dunia kuadhimisha siku ya Kiswahili duniani kwa mara ya Kwanza. Aidha, kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote, ninawakaribisha hapa Tanzania wageni wetu kutoka nje ya nchi, **Karibuni sana Tanzania, karibuni sana Dar es Salaam, mjisikie mko nyumbani!**

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;***
Leo ni siku muhimu sana kwa Taifa letu kwani tunapata nafasi ya kuadhimisha siku maalum ya lugha ya Kiswahili, yenye asili ya Kiafrika, ambayo chanzo na kitovu chake ni hapa nchini Tanzania. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipenda sana kujumuika nasi hapa katika Ukumbi huu, lakini haikuwezekana kutokana na majukumu mengine makubwa nje ya nchi na hivyo, amenituma nimwakilishe. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais ametuma ujumbe kwa njia ya Video ambayo naomba tuione na kuisikiliza kabla sijaendelea na hotuba yangu. Lakini pia, tumepokea salamu kutoka kwa Mheshimiwa Filipe Josinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji na Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, wakiungana nasi kuadhimisha siku ya Kiswahili Duniani, ambazo nazo naomba tuzisikilize pia.

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;***
Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na viongozi wetu hao, kutoka nchi jirani, kwa ujumbe waliotuletea kwa Kiswahili safi na fasaha! Naomba tuwashangilie tena kwa makofi. Sina budi sasa kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (MBW); Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, pamoja na Kamati ya Maandalizi na wadau wote wa Kiswahili, kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho ya leo na yale yote mliyofanya katika siku zote nne mlizokutana awali kuelekea kuadhimisha siku hii muhimu. Wote mliohudhuria hapa mtakubaliana nami kuwa maadhimisho

yamefana sana. Ninawapongeza kwa dhati wote waliofanikisha maadhimisho haya na wote mliohudhuria. **Hongereni Sana!**

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa na Ndugu Wananchi;***
Uamuzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) umekifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha saba (7) na lugha pekee ya Kiafrika kutambuliwa kama lugha rasmi katika Umoja wa Mataifa. Uamuzi huu haukufanywa kwa bahati mbaya bali ulizingatia ukubwa, ufasaha na kuenea kwa lugha hii duniani. Kama tulivyosikia, Kiswahili ni moja kati ya lugha 10 zinazozungumzwa zaidi duniani. Vilevile, inakadiriwa kuwa lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji zaidi ya milioni mia mbili (200,000,000). Ukiacha Tanzania, mataifa mengine ambayo lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji wengi, ni pamoja na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan Kusini, Somalia, Malawi, Zambia, Msumbiji, Komoro, Oman na Yemen. Aidha, lugha ya Kiswahili inatambulika kuwa miongoni mwa lugha rasmi za kazi katika Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Kwa nafasi hii, napenda kuwashukuru sana Waziri na Viongozi wenzake wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kusimamia na kutetea hoja iliyosababisha lugha ya Kiswahili kukubaliwa kuwa mojawapo ya lugha rasmi Umoja wa Mataifa na lugha rasmi za kazi Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Kipekee napenda kutambua mchango wa kizalendo uliotolewa na Mheshimiwa Balozi Prof. Kennedy Gastorn, Balozi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Innocent Shiyo, Balozi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Afrika, Mheshimiwa Samuel Shelukindo, Balozi wa Tanzania Nchini Ufaransa na timu ya wataalam waliohusika katika michakato husika.

Vilevile, lugha ya Kiswahili inafundishwa kama somo katika shule na vyuo mbalimbali duniani; aidha vyombo vya habari na mitandao mbalimbali ya kijamii inatumia lugha adhimu ya Kiswahili. Juhudi hizi za kutoa elimu kwa kutumia Kiswahili zilianza rasmi toka mwaka 1948 ingawa hata katika shughuli za elimu isiyo rasmi Kiswahili kilitumika toka mwaka 1929 kufundisha watu wachache kuwatumikia wakoloni. Serikali inatambua na kupongeza mchango mkubwa sana wa Taasisi mbalimbali zinazojikita katika uendelezaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili. Naomba nizitaje chache: TUKI, BAKITA, BAKIZA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Mhimili wa Mahakama pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama. Tunawapongeza Sana!

Hali kadhalika, kutokana na kukua kwa lugha ya Kiswahili hapa nchini, nyumba za Ibada pia zimeona umuhimu wa kutumia lugha hii adhimu katika kutoa mafundisho na pia kutafsiri nyaraka pamoja na vitabu mbalimbali vya dini kama Biblia Takatifu na Quran Tukufu.  Kiswahili kilitumika toka enzi za Umisionari hasa Waarabu wakieneza Uislamu na Wazungu wakieneza Ukristo.  Napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Viongozi wetu wa Dini, ambao ni pamoja na Hayati Askofu Mkuu Marko Mihayo, aliyesimamia kazi ya kutafsiri Biblia Takatifu katika lugha ya Kiswahili yenye Lahaja ya Kiunguja na hatimaye kuidhinisha ichapwe kwa mara ya kwanza, katikati ya miaka ya 1960; na Sheikh Abdullah Saleh al-Farsy, aliyetafsiri Quran Tukufu katika Lugha ya Kiswahili.

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;***
Uamuzi wa kuchagua tarehe 7 Julai ni wa heshima kubwa kwetu kwa sababu umefanyika kwa kuzingatia pia historia ya nchi yetu. Baadhi yenu mtakumbuka kuwa, tarehe 7 Julai mwaka 1954, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati huo akiwa Mwenyekiti wa TANU, alitangaza lugha ya Kiswahili kutumika katika kuunganisha wananchi kupigania uhuru. Maamuzi hayo ya kutumia Kiswahili yalikuwa ni msingi muhimu wa kuwaunganisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu suala la uhuru na kujitawala. Tangu hapo, Hayati Mwalimu Nyerere aliendelea kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Tarehe 10 Disemba mwaka 1962, Mwalimu Nyerere alihutubia Bunge la Kwanza la Tanganyika kwa lugha ya Kiswahili na tarehe 12 Februari 1963, lugha ya Kiswahili ilitangazwa rasmi kuwa lugha ya Taifa. Halikadhalika, kwa upande wa ndugu zetu wa Zanzibar, Kiswahili kilitumika kabla na baada ya mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Itakumbukwa, mwaka 1930 Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki wakati huo chini ya utawala wa Uingereza iliamua kuisanifisha lahaja ya kiunguja kuwa Kiswahili sanifu ambapo leo hii Kiswahili tunachotumia kinatokana na lahaja hiyo. Aidha, matumizi ya lugha ya Kiswahili Tanzania bara na Zanzibar ni moja ya sababu zilizochochea muungano wetu mwaka 1964, ambao umedumu kwa miaka 58 hadi leo.

Hakika tutaendelea kuwaenzi waasisi wa Taifa hili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume; na Viongozi wakuu wa Taifa letu waliofuatia, kwa kutambua umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika kuwaleta na kuwaweka watanzania na Waafrika pamoja. Aidha, tutaendelea kuwashukuru viongozi hawa kwa kuanzisha juhudi za makusudi kuhakikisha lugha hii inazungumzwa na watanzania wote na pia inavuka nje ya mipaka ya nchi yetu. Leo hii tunashuhudia dunia nzima ikiadhimisha siku ya Kiswahili kwa mara ya kwanza. Hii ni hatua kubwa sana na mafanikio ya kujivunia!

Hapa naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Joaquim Alberto Chissano, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji kwa kuwa mstari wa mbele kutangaza na kuihalalisha lugha hii adhimu barani Afrika. Kama Ujumbe wa Rais wetu ulivyosema, mwaka 2004, katika hotuba ya kuaga kama Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Mheshimwa Rais Chissano, alitumia lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza kuhutubia ili kuendeleza ahadi ya Umoja huo ya kukuza utambulisho na lugha za Kiafrika. Kitendo hiki kinatukumbusha pia kuwa lugha hii ilitumika na wapigania uhuru kama lugha ya mawasiliano na umoja katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Nimefahamishwa kuwa viongozi wetu wastaafu Mheshimiwa Joaquim Chissano na Mheshimiwa Samuel Daniel Nujoma, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Namibia walitegemewa kuwa hapa leo pamoja nasi, lakini wameshindwa kutokana na sababu zisizozuilika. Tunawaombea afya njema na umri mrefu wazee wetu hawa.

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa na Ndugu Wananchi;***
Ni dhahiri kuwa, lugha hii ya Kiswahili sasa imekuwa bidhaa, ajira na kiunganishi muhimu baina ya watumiaji. Kwa kutambua ukweli huo ndio maana Kauli mbiu ya maadhimisho haya inasema, "***Kiswahili kwa maendeleo na utangamano wa dunia."*** Ni Kauli mbiu muhimu katika zama hizi ambazo Serikali yetu inawahimiza wananchi wake kutafuta fursa mbalimbali zilizopo Duniani ambazo zitatuwezesha kupata kipato. Fursa hizo ni pamoja na shughuli za ukalimani, tafsiri, ufundishaji, uigizaji, uhariri na uandishi wa vitabu. Aidha, lugha ya Kiswahili ni nyenzo muhimu ya kujenga umoja na maelewano, kuwasiliana na kufanya biashara, ikiwa ni pamoja na utalii. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kutoa wito kwa Watanzania wote kushiriki katika kuzitambua na kuzitumia fursa zitokanazo na lugha ya Kiswahili kama Kauli mbiu ya maadhimisho haya inavyoeleza.

Ninawahakikishia kuwa, Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ipo tayari kushirikiana na Taasisi na wadau mbalimbali, kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili na kujenga ushawishi kwa nchi nyingine kuingiza Kiswahili katika mitaala yao ili kuendelea kusambaza lugha hii adhimu kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Na kudhihirisha hilo, leo hapa tumeshuhudia utiaji saini wa Hati ya Makubaliano ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi Afrika Kusini. Hii ni fursa kubwa sana kwetu. Sanjari na haya makubaliano, Mkakati huu wa Taifa wa kubidhaisha Kiswahili tuliouzindua leo, pamoja na mambo mengine, unalenga kuwatangaza wataalamu wetu wa lugha ya Kiswahili katika masoko ya kimataifa na kuitangaza tasnia ya uchapishaji pamoja na kazi za uchapishaji kitaifa na kimataifa. Serikali inatekeleza haya yote na kuthibitisha kwa vitendo

kuwa Kiswahili ni chetu. Hivyo, napenda nitoe rai kwa Wataalamu wa Kiswahili kutumia utaalamu na ubunifu wenu kukipeleka Kiswahili huko duniani ili tupate matunda ya ajira na kukuza uchumi wetu.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***
Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la upotoshaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamii, hususan vijana. Aidha, kumekuwa pia na tatizo la kutotumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na badala yake kutumia maneno yasiyo rasmi au kuchanganya kiswahili na maneno ya lugha nyingine. Hivyo, ni vema nitumie nafasi hii kusisitiza na pia kutoa wito kwenu wataalamu, mabingwa na wapenzi wa lugha ya Kiswahili kuendelea kuongea Kiswahili fasaha na kuandika vitabu vya taaluma mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hali ilivyo sasa, ni dhahiri kuwa kuna uhitaji mkubwa wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, hatuna budi kukidhi haja hii. Ninawapongeza wale wote wanaotumia mitandao ya kijamii na TEHAMA kwa ujumla kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili. Katika ulimwengu wa sasa ni dhahiri kuwa mitandao ya kijamii pamoja na tovuti mbalimbali zina mchango mkubwa sana katika kueneza, kufundisha na kukifanya Kiswahili kuwa sehemu ya maendeleo ya teknolojia, jambo ambalo litachochea lugha yetu isambae kwa haraka na kwa ufasaha.

Vilevile, napenda nitumie fursa hii kupongeza Balozi zetu nje ya nchi, zilizoadhimisha siku hii ya Kiswahili Duniani kwa kufanya makongamano na kuandaa midahalo. Nimeona video na vipeperushi mbalimbali kwenye mitandao vikihamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mataifa mbalimbali duniani. **Hongereni kwa kazi nzuri!**

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;***
Wakati najiandaa kuja kuzungumza katika maadhimisho haya leo, nilimkumbuka mshairi na mtunzi wa vitabu vya Kiswahili Hayati Shaaban Robert ambaye alitoa mchango mkubwa sana katika ukuzaji wa fasihi ya lugha ya Kiswahili. Katika shairi lake "***Titi la Mama li Tamu***" lililochapishwa katika kitabu chake cha mkusanyiko wa mashairi cha *"Pambo la Lugha."* Shaaban Robert, anaulinganisha utamu wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili na *Titi la mama* kwa mtoto wake, kwa kusema:

***"Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa,***
***Kiswahili naazimu, sifayo inayofumbwa,***
***Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,***
***Toka kama chemchemu, furika palipozibwa,***
***Titi la mama litamu, jingine halishi hamu.***

Naamini Sote tunakubaliana kuwa lugha yetu ya Kiswahili ni tamu kama titi la mama lilivyo kwa mtoto. Hivyo, ni wajibu wetu kuendelea kuienzi lugha hii adhimu kwa kuendeleza matumizi yake sahihi na kuonesha umuhimu wake kwa wasioifahamu hata waone hamu ya kuitumia kama alivyoandika Shaaban Robert. Kwa nafasi hii, napenda pia kuwashukuru washairi wengine nguli kama Saadan Abdul Kandoro, Mohamed Seif Khatib na Sheikh Kaluta Amri Abeid kwa mchango wao wa kueneza Kiswahili. Vile vile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa awamu ya pili; pamoja na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari na Wahadhiri kutoka Vyuo Vikuu kwa kufundisha Kiswahili.

Aidha, kupitia hadhara hii ninapenda niwahimize pia vijana kuwa na tabia ya kusoma na kuandika vitabu vya Kiswahili na kuwa mstari wa mbele kuiendeleza lugha hii. Tunataka kuwa na akina Shaaban Robert, Mohamed Seif Khatib na Shafi Adam Shafi wengi, ambao watasomwa vizazi na vizazi duniani. Hii ni fursa kwenu, changamkeni!

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa na Ndugu Wananch;***
Ili kuendelea kukuza matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili nchini na duniani, napenda kusisitiza kuwa hatuna budi kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia aliyoyatoa, akiwa Makamu wa Rais wakati wa kufungua maadhimisho ya siku ya Kiswahili kitaifa yaliyofanyika tarehe 19 – 20 Januari 2021, Jijini Dodoma. Wizara zinazohusika na Utamaduni SMT na SMZ, ni muhimu zibaini maeneo ambayo bado Kiswahili hakitumiki ipasavyo ili hatua zaidi zichukuliwe, hususan kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha. Aidha, Mabaraza ya Kiswahili yaandae mikakati mahususi ya kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ili Serikali iyawezeshe kwa kuyapatia wataalam na kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya miradi ya Kiswahili ya mabaraza haya.

Sambamba na maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais, napenda pia kuelekeza kama ifuatavyo:

i. **Jambo la kwanza,** Wizara zenye dhamana ya Elimu zifanyie kazi matokeo ya tafiti nyingi ambazo zimefanyika kuhusu lugha ipi inafaa kufundishia ili Serikali ifanye uamuzi na hatimaye watoto na vijana wa Kitanzania waanze kujifunza kwa lugha yao tamu ya kiswahili kuanzia shule ya awali hadi Chuo Kikuu;

ii. **Jambo la pili,** Wizara na taasisi za Serikali ziendelee kutekeleza maagizo ya Serikali yaliyokwishatolewa kuwa: Nyaraka za mawasiliano za Wizara na Idara zake ziwe kwa lugha ya kiswahili na kwamba mikutano, warsha, semina, mijadala ya umma na dhifa ziendeshwe kwa Kiswahili. Vilevile, majina ya barabara, mitaa, mabango, fomu za usaili na maelekezo ya matumizi ya dawa zote na bidhaa na huduma pia viandikwe kwa Kiswahili;

iii. **Jambo la tatu,** Taarifa za miradi na mikataba inayohusu wananchi ni lazima ziwe kwa lugha ya Kiswahili, na isiwe katika lugha za kigeni pekee, ili wananchi waelewe kila jambo muhimu katika ustawi wa maisha yao;

iv. **Jambo la nne,** Sheria na Kanuni ambazo bado hazijatafsiriwa, zitafsiriwe na wizara na taasisi zinazosimamia sheria na kanuni hizo, kwa kushirikiana na mabaraza ya Kiswahili, wataalamu wengine wa Kiswahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

v. **Jambo la tano,** Vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili vihakikishe vinatumia Kiswahili fasaha na sanifu, huku vikizingatia kwa dhati sarufi ya Kiswahili. Aidha, pale anaposhirikishwa mtu anayeongea lugha isiyokuwa Kiswahili, chombo cha habari kinachohusika kitoe tafsiri ya maneno yasiyo ya Kiswahili ili wananchi waelewe kilichozungumzwa;

vi. **Jambo la sita,** napenda nisisitize agizo lililotolewa kwa Balozi zote za Tanzania, kuanzisha vituo vya kujifunzia lugha ya Kiswahili. Hapa, napenda niziagize Balozi ziwatumie wataalamu wa lugha ya Kiswahili waliosajiliwa kwenye kanzidata za BAKITA na BAKIZA;

vii. **Jambo la saba,** BAKITA kwa kushirikiana na BAKIZA muendelee kuwa wabunifu katika kuzalisha misamiati ya Kiswahili ili kuendana na kasi ya maendeleo ya kisayansi na teknolojia;

viii. **Jambo la Nane na la mwisho**, Wizara na taasisi husika mhakikishe mfumo wa kufundisha kiswahili kwa wageni kwa njia ya mtandao (**Swahili Prime**) unatumika kikamilifu.

***Waheshimiwa Viongozi, wageni waalikwa, Washiriki Wote na Ndugu Wananchi;***

Napenda nimalizie hotuba hii kwa kuwakumbusha wananchi wote wa Tanzania kuwa tarehe 23 Agosti 2022 ni siku ya Sensa ya Watu na Makazi. Nawaomba

wananchi wote wajitokeze kuhesabiwa na kutoa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

Baada ya kusema hayo, nawatakia Watanzania na wazungumzaji wote wa kiswahili siku njema ya **Kiswahili Duniani, 2022.**

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Ibariki Lugha yetu adhimu ya Kiswahili,

**Asanteni kwa kunisikiliza!**